# AckySHINE.com

# Utaratibu wa Mkristo Mkatoliki Kanisani

By DIN - Melkisedeck Leon Shine · February 24, 2020

Mafundisho ya Msingi ya Kanisa Katoliki: Makala za Katoliki · #Karibu AckySHINE · #Katoliki: Ibada · #Katoliki: Kanisa Katoliki

Ninapoingia kanisani nachovya maji ya baraka na kusema;"Unitakase Ee Bwana mimi na uovu wangu wote, ili nipate kustahili kushiriki ibada takatifu' Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu" Amina!

Ninapiga goti huku nikisema"Mungu wangu na Bwana wangu"

??Nikiinuka nasema

"Nitakusifu na kukuabudu katika Ekaristi takatifu"

??Naenda mpaka kwenye bench, napiga magoti au nakaa nikiwa mimeinamisha kichwa (kama mabenchi yameisha nabaki nimejisimamia) huku nikitoa nia yangu ya kusali misa siku hiyo, mfano

"Ee Mungu, ninaungana nawe na jeshi lote la mbinguni, pamoja na Mama Bikira Maria, nikiwa na nia ya kumwombea mama yangu ambaye ni mgonjwa, jirani yangu ambaye mpaka sasa hatuelewani na pia familia yetu ambayo haina amani, Mungu kupitia misa hii rejesha hali ya mama yangu, rejesha uelewano na jirani yangu, na pia rejesha amani ya familia yetu pamoja na familia zote ambazo hazina amani"

??Ninaendelea na misa na Kushiriki litrujia kikamilifu

??Wakati wa komunyo nikikumbuka kuwa nina dhambi kubwa huwa nakominika kwa sala ya tamaa wala siendi mbele, huwa najikalia tu kwenye bench naangalia wenye moyo safi wanaenda mbele kumpokea Yesu (Kweli huwa najisikia wivu sana, itanibidi katikati ya wiki nifanye kitubio ili nisikae tena)"

??Mwisho wakati wa kuondoka nachovya maji ya baraka nikisema

"Unilinde Ee Mwenyezi Mungu, nikapate kuwa mfano katika jamii yangu, na nikushuhudie katika matendo yangu"(Hapo nachovya maji ya baraka na kufanya ishara ya msalaba) "Kwa jina la Baba na la Mwana na la Roho Mtakatifu, amina"

Usiku mwema wapendwa. Malaika awalinde